




WIZARA YA UJENZI  
WAKALA YA BARABARA TANZANIA



**TAARIFA YA MPANGO KAZI WA TATHMINI YA ATHARI YA MAZINGIRA KWA JAMII KWA MRADI WA UKARABATI WA BARABARA YA LUTUKIRA – SONGEA (100 km) NA BARABARA YA MCHEPUKO WA SONGEA (16 km) NA MTWARA – MINGOYO – MASASI (km 200) MKOANI RUVUMA, LINDI NA MTWARA**

Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS) kwa niaba ya Wizara ya Ujenzi inakusudia kuanza utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa barabara ya Lutukira – Songea (km 100) na Barabara ya mchepuko wa Songea (km 16) na Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200) kwa kiwango cha lami, Mkoani Ruvuma, Lindi na Mtwara kwa kutumia fedha za mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia.

Mpango Kazi wa tathmini ya athari ya mazingira kwa jamii umeandaliwa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 na muundokazi wa Mazingira na Jamii wa Benki ya Dunia,

Kwa Tangazo hili, Wakala ya Barabara inaweka wazi mpango kazi huo kwa Umma na inawaalika wadau na jamii kwa ujumla kuupitia kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa mradi huo.

Aidha, Umma unaweza kusoma mpango kazi huo kwenye Tovuti ya TANROADS:  
[www.tanroads.go.tz](http://www.tanroads.go.tz) na kwenye Ofisi zifuatazo:

1. Wakala ya Barabara (TANROADS),  
S.L.P 11364,  
10 Shaaban Robert Road/Garden Avenue Junction,  
**Dar es Salaam.**  
Email:[tanroadshq@tanroads.go.tz](mailto:tanroadshq@tanroads.go.tz)
2. Ofisi ya Wakala ya Barabara  
Mkoa wa Ruvuma  
S.L.P 31,  
**Ruvuma.**  
Email: [rm - ruvuma@tanroads.go.tz](mailto:rm - ruvuma@tanroads.go.tz)